

Virusi vya Mfumo wa Kupumua vya Syncytial (RSV) Kingamwili ya Kuzuia: *Unachohitaji Kujua*

Kwa nini upate chanjo ya Kingamwili ya Kuzuia ya RSV?

Kingamwili ya kuzuia ya virusi vya mfumo wa kupumua vya syncytial (Respiratory Syncytial Virus, RSV) inaweza kuzuia ugonjwa mkali wa mapafu unaosababishwa na RSV.

RSV ni virusi vya kawaida vya mfumo wa kupumua ambavyo kwa kawaida husababisha dalili ndogo zinazofanana na mafua lakini zinaweza kuathiri mapafu pia. Dalili za maambukizi ya RSV zinaweza kujumuisha kutiririka kamasi, kupungua kwa hamu ya kula, kukoho, kupiga chafya, joto kali, au kukokota pumzi.

Mtu ye yote anaweza kuambukizwa na RSV, na karibu watoto wote hupata maambukizi ya RSV wanapokuwa na umri wa miaka 2. Huku watoto wengi wanapona maambukizi ya RSV kwa wiki au mbili, maambukizi ya RSV yanaweza kuwa hatari kwa watoto wachanga na baadhi ya watoto wadogo, na kusababisha ugumu wa kupumua, viwango vya chini vya oksijeni, na upungufu wa maji mwilini. Nchini Marekani, RSV ndiyo sababu ya kawaida zaidi ya bronkiolitis (kuvimba kwa njia ndogo za hewa katika mapafu) na nimonia (maambukizi ya mapafu) kwa watoto walio na umri wa chini ya mwaka 1. Watoto wanaokuwa wagonjwa kutokana na RSV wanaweza kulazwa hospitalini, na wengine wanaweza hata kufa.

Kingamwili za Kuzuia za RSV

Kingamwili ya kuzuia ya RSV (jina la jumla nirsevimab, jina la biashara Beyfortus) ni sindano ambayo huzuia ugonjwa mkali wa RSV kwa watoto wachanga na watoto wadogo. Kingamwili ni protini ambazo mfumo wa kinga ya mwili hutumia kupigana na vijidudu hatari. Kama chanjo za asilia, kingamwili za kuzia ni chanjo ambazo hutoa ulinzi dhidi ya pathojeni maalum. Huku zote zikiwa chanjo, namna ambavyo zinatoa kinga ni tofauti. Nirsevimab ni chanjo ambayo hutoa kingamwili moja kwa moja kwa mpokezi. Chanjo za asilia ni chanjo ambazo huchochea mfumo wa kinga ya mwili wa mpokeaji kutoa kingamwili.

Watoto wachanga wanaozaliwa wakati wa msimu wa RSV (kwa kawaida msimu wa kuchipua) wanafaa kupokea dozi moja ya Chanjo ya RSV ndani ya wiki 1 baada ya kuzaliwa. Watoto wengi wachanga amba mama zao walipokea chanjo ya RSV hawahitaji kupokea nirsevimab, pia. Zote mbili hulinda watoto wachanga dhidi ya RSV kali kwa kutoa kingamwili, ama kutoka kwa mama hadi kwa mtoto mchanga au moja kwa moja kwa mtoto mchanga. Watoto wengi wachanga watahitaji tu ulinzi kutoka kwa chanjo ya uzazi ya RSV au nirsevimab (sio zote mbili). Hata hivyo, kunaweza kuwana hali ambapo nirsevimab itapendekezwa kwa mtoto mchanga baada ya mama kupokea chanjo ya RSV.

Watoto waliozaliwa nje ya msimu wa RSV amba wana umri wa chini ya miezi 8 wanapaswa kupokea dozi moja ya Chanjo ya RSV muda mfupi kabla ya msimu wao wa kwanza wa RSV (kwa kawaida msimu wa vuli), lakini watoto wachanga walio na umri wa chini ya miezi 8 amba bado hawajapokea dozi wanaweza kupokea dozi wakati wowote wakati wa msimu.

Baadhi ya watoto wachanga na watoto wadogo walio katika hatari kubwa ya kupata ugonjwa mkali wa RSV wanaweza kuhitaji dozi moja ya kingamwili ya RSV kabla au wakati wa msimu wao wa pili wa RSV.

Kingamwili za kuzuia za RSV zinaweza kutolewa wakati mmoja na chanjo zinazopendekezwa mara kwa mara kwa watoto wachanga na watoto wadogo.

Zungumza na mto huduma za afya wako

Mwambie mto huduma wako wa afya ikiwa mtu anayepata kingamwili ya kuzuia ana:

- Historia ya athari mbaya za mizio kwa kingamwili ya kuzuia RSV (nirsevimab) au sehemu zake zozote,
- Ugonjwa wa kutokwa na damu, au
- Ugonjwa wa wastani au mbaya sana.

Katika baadhi ya visa, mto huduma za afya wa mtoto wako anaweza kuamua kuahirisha chanjo za kingamwili za RSV hadi katika ziara ya baadaye.

Watu walio na ugonjwa mdogo, kama vile mafua, wanaweza kupokea kingamwili ya kuzuia ya RSV kwa usalama. Watu ambao ni wagonjwa kwa wastani au wagonjwa vibaya wanapaswa kwa kawaida kungojea hadi wapone.

Mto huduma wako wa afya anaweza kukupa habari zaidi.

Hatari za mmenyuko kwa kingamwili za kuzuia RSV

Baada ya kupokea kingamwili ya kuzuia ya RSV, mtoto wako anaweza kuwa na maumivu ya muda, wekundu, uvimbe ambapo sindano ilitolewa, au upele.

Kama ilivyo na dawa yoyote ile, kuna uwezekano mdogo ambao Chanjo ya RSV inaweza kusababisha mmenyuko mkali wa mizio, majeraha mengine mabaya, au kifo.

Mmenyuko wa mizio unaweza kutokea baada ya mtoto wako kuondoka hospitalini au kliniki. Ikiwa utaona dalili za mmenyuko mkali wa mizio (kwa mfano, mabaka, kuvimba uso na koo, matatizo ya kupumua, moyo kupiga haraka, kizunguzungu, au udhaifu), piga simu 9-1-1 na umpeleke mtoto wako kwenye hospitali iliyo karibu.

Mpigie simu mto huduma wako wa afya ikiwa utaona dalili nyingine zinazokupatia wasiwasi.

Je, itakuwaje ikiwa kuna tatizo mbaya sana?

Ikiwa mtoto wako alipokea kingamwili ya kuzuia ya RSV bila kupatachanjo kwa wakati mmoja, na unashuku athari mbaya, wewe au mto huduma wako wa afya mnawenza kuwasilisha ripoti kuitia <https://www.fda.gov/medwatch> au kwa simu katika 1-800-FDA-1088.

Ikiwa mtoto wako alipokea kingamwili ya kuzuia ya RSV wakati mmoja na unashuku athari mbaya, wewe au mto huduma wako wa afya mnawenza kuwasilisha ripoti kwa [Mfumo wa Kuripoti Matukio Mabaya ya Chanjo \(Vaccine Adverse Event Reporting System, VAERS\)](#) <https://vaers.hhs.gov/> au kupiga simu katika 1-800-822-7967.

Kwenye ripoti yako, elezea kwamba mtoto wako alipokea Chanjo ya RSV wakati mmoja na chanjo.

Kumbuka: MedWatch na VAERS ni za kuripoti miitikio pekee.

Wafanyakazi wa MedWatch na VAERS hawatoi ushauri wa kimatibabu.

Je, ninawezaje kujifunza mengi zaidi?

- Muulize mto huduma wako wa afya.
- Piga simu kwa idara ya afya ya eneo au ya jimbo lako.
- Tembelea tovuti ya U.S. Food and Drug Administration katika [Drugs@FDA: Dawa Zilizoidhinishwa-FDA](#).
- Wasiliana na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (Centers for Disease Control and Prevention, CDC):
 - Piga simu 1-800-232-4636 (1-800-CDC-INFO) au
 - [Tembelea tovuti ya CDC](#) <https://www.cdc.gov/rsv/about/prevention.html>

